# JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA SAME

FAHARI YA SAME

Maendeleo Daima

Toleo la Machi 2024 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022

## FANYENI TAFITI KUPATA NISHATI MBADALA YA KUPIKIA-DKT. MPANGO



*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.Phillip Mpango akimwagilia mti baada ya kuuotesha kwenye viwanja vya shule ya Sekondari Same kama sehemu ya maadhimisho ya siku ya Misitu Duniani na siku ya Upandaji Miti Kitaifa.*

Makamu wa Rais, Mhe.Dk. Philip Isdor Mpango ameitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kupitia Taasisi zake na wadau wa Mazingira kufanya tafiti za namna ya kupata teknolojia za kisasa zitakazopunguza matumizi ya mkaa na kuni kama nishati ya kupikia ili kunusuru uharibifu wa Misitu.

Akizungumza Wilayani Same, Kilimanjaro Machi 21,2024 katika Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Upandaji wa Miti Kitaifa, Dkt. Mpango amesema sekta ya Misitu nchini Tanzania bado inakabiliwa na changamoto nyingi, ikiwemo uharibifu mkubwa wa maeneo ya Hifadhi, hali inayochochea mabadiliko ya tabia nchi.

Amesema matumizi ya nishati chafu (kuni na mkaa) hapa nchini yameendelea kuwa kichocheo kikubwa cha ukataji holela wa miti na uharibifu wa Hifadhi za misitu, changamoto ambayo inabidi kukabiliwa haraka iwezekanavyo.

“Takwimu zinaonyesha kuwa, katika kila kaya 10 nchini Tanzania, kaya 9 zinatumia nishati ya kuni na mkaa, hii ni changamoto kubwa ambayo lazima wizara husika ishirikiane na Taasisi zake na wadau katika kuikabili,” alisema.

Ameitaka Wizara ya Maliasili na Utalii, TAMISEMI, Chuo cha Olmotonyi , Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) kushirikiana kwa dhati na wadau wengine katika kubuni teknolijia ya kisasa itakayosaidia katika kudhibiti uharibifu wa rasilimali za misitu nchini Tanzania.

“Tafiti na teknolojia hizo ni lazima zilenge katika jitihada za kuvumbua nishati mbadala nyepesi na rafiki kwa mazingira, lakini pia, tunahitaji kuwa na teknolojia rafiki itakayosaidia zao la tumbaku kukaushwa bila uharibifu wa mazingira,” Dkt. Mpango aliagiza.

Makamu wa Rais amezitaka Wilaya na Halmashauri zote nchini kutenga maeneo mengi ili kuruhusu miti kupandwa kwa wingi zaidi, huku akiwaelekeza Wakurugenzi wa Majiji ,Miji na Halmashauri hapa nchini kuanzisha bustani nzuri za miti kwa ajili ya mapunziko na mazoezi.

Awali akimkaribisha mgeni rasmi, Waziri wa Maliasili na Utalii, Mhe. Angellah Kairuki (Mb) alisema kuwa Sekta ya Misitu inachangia asilimia 3.5 ya pato la Taifa, ikiwa pamoja na asilimia 10 ya ajira kwa Watanzania.

Waziri Kairuki alisema dhumuni la Maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Upandaji Miti Kitaifa, pamoja na mambo mengine ni kuhamasisha umma juu ya umuhimu wa upandaji na utunzaji miti, na kuongeza, kauli mbiu ya Maadhimisho ya mwaka huu ya ‘Misitu na Ubunifu’ kauli inaonyesha dhamira njema ya Serikali katika kukuza sekta ya misitu.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Mhe. Nurdin Babu amesema Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Upandaji Miti Kitaifa ni siku muhimu sana kwa Taifa na wakazi wa Kilimanjaro, na Wilaya ya Same na Taifa zima kwa ujumla.

Amesema mpaka sasa Mkoa wa Kilimanjaro umefanikiwa kupanda zaidi ya miti milioni 8, na kwamba wameweka mikakati mbalimbali endelevu ya kuhakikisha miti hiyo inatunzwa vyema kwa kuwachukulia hatua kali za kisheria dhidi ya wafugaji wenye tabia ya kulisha mifugo kwenye maeneo ya Hifadhi.

## MAELEKEZO YA MAKAMU WA RAIS DKT.PHILIP MPANGO ALIYOYATOA SIKU YA MISITU DUNIANI.




*Waziri wa Maliasili ya Utalii Mheshimiwa Angellah Kairuki akikabidhi Tuzo ya Shukrani kwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.Phillip Mpango kutokana na uongozi wake imara kwa Watanzania, ni katika maadhimisho ya siku ya Misitu Duniani na upandaji miti Kitaifa*

1. Mradi Mkubwa wa maji wa Same-Mwanga-Korogwe (SMK) ukamilike na kuanza kutoa huduma ifikapo Juni 2024.

2.Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya zianzishe maeneo ya uhifadhi wa Misitu katika maeneo yao.

3.Wizara ya Maliasili na Taasisi zake kwa kushirikiana na wadau wafanye tafiti ili kupata nishati mbadala kupunguza matumizi ya kuni na mkaa kama nishati ya kupikia maana kaya 9 kati ya 10 hapa Tanzania bado zinategemea mkaa na kuni kupikia .

4. Wakala wa Misitu Nchini (TFS) wahakikishe kila Halmashauri inakuwa na vitalu vya miti.

5.Kila Wilaya ihakikishe inadhibiti matumizi ya Msumeno Mnyororo (Chainsaw) katika uvunaji wa miti ili kuzuia uvunaji holela wa miti.

6.Majiji. Manispaa, Miji na Halmashauri za Wilaya zijifunze fursa zilizopo kwenye biashara ya hewa ya ukaa (Carbon).

7. Wekeni ubunifu katika Uendelezaji na Utunzaji wa Misitu ili kuzuia athari za kimazingira.

8.Wizara ya Maliasili na Utalii ifanye Mapitio juu ya viwango vinavyolipwa kwa wananchi wanaoathiriwa na wanyama waharibifu.

9.Jeshi la Polisi endeleeni kupambana na dawa za kulevya ikiwemo udhibiti wa kilimo cha Mirungi hasa katika Wilaya hii ya Same.

10.Wananchi washiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa 2024 kwani Maendeleo ya haraka yanategemea aina ya Kiongozi utakayemchagua.,na wananchi wenye sifa wajitokeze kugombea.

11.Kisima kichimbwe Same Sekondari ili kukabiliana na changamoto ya maji.




*Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.Phillip Mpangoakitembelea mabanda ya maonyesho ya bidhaa za Misitu kwenye viwanja vya shule ya Sekondari Same.*

# ZIARA YA MAKAMU WA RAIS DKT. MPANGO ILIVYOLETA NEEMA SAME SEKONDARI



*Uchimbaji wa Kisima ukiendelea kwenye shule ya Sekondari Same, uchimbaji huo umefanika kufuatia agizo la Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt.Phillip Mpango alilolitoa shuleni hapo.*

Ujio wa Makamu wa Rais Mheshimiwa Dkt.Philip Mpango kwenye Wilaya ya Same umeleta neema kwa Shule ya Sekondari Same kuchimbiwa kisima cha maji baada ya shule hiyo kukosa maji ya uhakika kwa muda mrefu.

Mkuu shule hiyo Mwl.Abeidnego Mbuki amesema tayari kisima kimeshachimbwa shuleni hapo na zinazoendelea ni taratibu za maabara za upimaji wa maji hayo ili yaanze kutumika.

“Tunashukuru agizo la Makamu wa Rais Dkt Philip Mpango limeshatekelezwa na tunachosubiri ni kukamilika kwa taratibu kadhaa ili wanafunzi waanze kunufaika na huduma ya uhakika ya maji” alisema Mwl.Mbuki.

Dkt.Mpango alifika kwenye shule ya Sekondari Same kuotesha mti kama sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na siku ya upandaji miti kitaifa ambapo pia alipata ,muda wa kuongea na wanafunzi wa shule hiyo kongwe yenye wanafunzi wa kidato cha tano na sita wapatao 920 ambayo ilianzishwa mwaka 1952.

Wanafunzi hao walitumia fursa hiyo vizuri ambapo waliwasilisha kilio chao cha ukosefu wa maji ya uhakika jambo linalosababisha wakati mwingine wapeane zamu za kuoga.

Akitoa neno la shukrani kwa Makamu wa Rais kufika na kuotesha mti shuleni hapo, Mwanafunzi wa kidato cha sita Joshua Mwakijangala alimuomba Makamu wa Rais kusaidia upatikanaji wa maji shuleni hapo.

“Mheshimiwa Makamu wa Rais tumefurahi sana wewe kufika hapa shuleni kwetu,hapa shuleni tuna changamoto ya upatikanaji wa maji tunaomba utusaidie tupate maji ya uhakika” aliomba Mwanafunzi huyo.

Akijibu maombi hayo Makamu wa Rais Mheshimiwa Mpango alimwagiza Waziri wa maji Juma Aweso aliyekuwepo kwenye msafara huo kuhakikisha kuwa visima vinachimbwa shuleni hapo ambapo Waziri Aweso aliahidi utaratibu wa kuchimba kisima utaanza Machi 22,2024.

## WAZIRI MKUU MAJALIWA AZINDUA MBIO ZA MWENGE WA UHURU 2024-KILIMANJARO



*Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Kassim Majaliwa akiwasha Mwenge wa Uhuru 2024 kwenye viwanja vya Chuo Kikuu cha Ushirika Mjini Moshi, April 02 mwaka huu.*

Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa amezindua rasmi Mbio za Mwenge wa Uhuru 2024 katika viwanja vya Chuo cha Ushirika Mjini Moshi, Mkoani Kilimanjaro.

Akizindua Mbio hizo April 02 mwaka huu, Waziri Mkuu aliwataka wakimbiza Mwenge kitaifa kuhakikisha kuwa wanahubiri agenda za Taifa katika kila eneo ambalo Mwenge utafika.

"Hakikisheni mnahubiri agenda za Kitaifa kila mnakopita, hamasisheni wananchi kushiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, kemeeni vitendo vya rushwa maana wote tunatambua kuwa rushwa ni adui Wa haki" alisema Mheshimiwa Majaliwa.

Mheshimiwa Majaliwa aliwataka wakimbiza Mwenge kuhakikisha kwamba wanakemea rushwa katika maeneo yote wanayopita kwani rushwa ni adui wa haki lakini pia waendelee kuwahimiza wananchi kujilinda dhidi ya maambukizi ya VVU.

“Baadaye mwakani tutakuwa na chaguzi za Serikali za Mitaa hivyo katika maeneno yote mwenge utakapopita wananchi wahamasishwa kushiriki chaguzi hizo ikiwa ni pamoja na kujitokeza kugombea nafasi mbali mbali na pia kuchagua viongozi bora.

Waziri Mkuu aliwataka wakimbiza Mwenge kitaifa kukemea matumizi ya Dawa za kulevya ambapo alionya vijana kuepuka matumizi ya Dawa za kulevya.

"Kuna kitu kinaitwa cha Arusha,Vijana achaneni kabisa na hivi vitu kwani kitawapotezea mwelekwo Wa maisha"alionya Majaliwa.

Aidha amewataka wakimbiza Mwenge Kitaifa kutofumbia macho mapungufu watakayoyaona kwenye Miradi mbalimbali badala yake watoe taarifa ili hatua stahili ziweze kuchukuliwa.

Akizungumza baada ya kupokea Mwenge wa Uhuru 2024 Kiongozi wa mbio za Mwenge Kitaifa 2024 Ndg. Godfrey Elihakim Mnzava aliahidi kufikisha ujumbe huo sehemu zote ambazo Mwenge wa Uhuru utakimbizwa.

Mwenge wa Uhuru mwaka huu umebebwa na kaulimbiu isemayo "Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu"

## IDADI WA WATALII YAONGEZEKA NCHINI-WAZIRI KAIRUKI



*Watalii wakimwangalia Faru mweusi kwenye hifadhi ya Taifa Mkomazi, Wilayani Same Mkoani Kilimanjaro (picha kwa hisani ya Mkomazi )*

Idadi ya watalii waliotembelea Tanzania imeongezeka kutoka watalii 1,400,000 mwaka 2022 na kufikia 1,881,823 mwezi Februari 2024 ambao wameweza kuliingiza Taifa dola za kimarekani bil.3.5.

Hayo yamebainishwa na Waziri wa Maliasili na Utalii Mhe.Angellah Kairuki wakati akizindua Tamasha kubwa la Utalii Wilayani Same (Same Utalii Festival-SUF) Feb 23,2024.

Akizindua Tamasha hilo la siku tatu linalojulikana kama Same Utalii Festival Waziri Kairuki alisema ongezeko hilo la watalii limechangiwa na jitihada za Mhe.Rais Samia Suluhu kutangaza utalii kupitia filamu ya Royal Tour.

"Tutakua wachoyo wa fadhila iwapo hatutamshukuru Mheshimiwa Rais kusaidia ongezeko la watalii kupitia filamu ya Royal Tour"alisema Mhe.Kairuki.

Mheshimiwa Waziri amewataka pia wananchi wa Tanzania kushiriki kufanya Utalii katika maeneo mbalimbali ya utalii hapa nchini ili kuendelea kutangaza vivutio vya utalii hapa nchini.

"Tusisubiri wazungu tu kuja kutembelea vivutio vyetu vya Utalii,tuanze sisi ili wazungu wafuate"alisema Mheshimiwa Waziri.

Aidha Waziri Kairuki alitoa wito kwa kampuni za Utalii na hoteli zinazopokea watalii kutoa huduma bora ili watalii hao waweze kuvutiwa na kutembelea tena Tanzania.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha kuwa nchi imetembelewa na watalii milioni tano ifikapo 2025.

Akizungumza katika Uzinduzi huo, Mkuu wa Wilaya ya Same Mhe.Kasilda Mgeni alisema lengo la kuandaa Tamasha hilo ni kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo Wilayani Same ili kukuza uchumi wa wananchi na kuongeza pato la Serikali.

"Tamasha hili la Same Utalii Festival litakuwa linafanyika kila mwaka, tunaamini itasaidia sana kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo katika Wilaya hii"alisema Mheshimiwa Kasilda.

Katika Tamasha hilo wageni walifanikiwa kutembelea Hifadhi ya Taifa Mkomazi, Mlima Kidenge na Hifadhi ya Msitu wa asili Chome.

Meneja wa Tamasha la Same Utalii Festival (SUF) Bw.Amon Mchomvu ameshukuru jitihada za Serikali katika kuinua Uchumi wa Wilaya ya Same kwa njia ya Utalii.

“Kwakweli Tamasha hili limefana sana na limechagia uchumi wa wafanyabiashara katika eneo letu” alisema Mchomvu.

## WANANCHI WA RUVU WANAOISHI ENEO LA PORI TENGEFU WATAKIWA KULIMA MAZAO YA MUDA MFUPI




*Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Jerry Slaa akisalimiana na viongozi wa Mkoa na wa Wilaya ya Same alipowasili Wilayani Same kwa ziara ya siku moja mwishoni mwa Mwezi Januari 2024.*

Waziri wa Ardhi Mheshimiwa Jerry Slaa amewaruhusu wananchi wa Kata ya Ruvu ambao wanaishi kwenye eneo la Pori Tengefu kuendelea kulima mazao yanayokomaa muda mfupi wakati Serikali ikilitafutia ufumbuzi suala lao la kuishi kwenye eneo la Pori Tengefu.

Akizungumza alipofanya ziara kwenye Kata ya Ruvu Mheshimiwa Slaa aliwataka wananchi hao kufuata maelekezo ya Serikali yanayowazuia kufanya maendelezo yoyote katika eneo hilo hadi pale Serikali itakapokuja na maelekezo rasmi.

"Hili eneo ni pori Tengefu na Serikali imeshatoa maelekezo mbalimbali hapa hasa zuio la kufanya maendeleo ya kudumu ikiwemo kujenga nyumba za kudumu,nni vema maelekezo ya Derikali yakafuatwa ila suala la kulima mimi nawaruhusu mlime mazao ya muda mfupi" alise Waziri Slaa

Waziri Slaa alisema maamuzi kuhusu eneo hilo yanapaswa kuamuliwa na Mawaziri kutoka sekta nane na Mwenyekiti wa kikao hicho ni Waziri wa Ardhi hivyo ameahidi kuitisha kikao cha Mawaziri hao mapema mwezi February 2024 na baada ya kikao hicho atawasilisha majibu rasmi kwa wananchi wa Ruvu.

"Mama Samia aliponiteua alinielekeza kuwa jambo asilolitaka ni kusababisha taharuki kwa wananchi, hivyo niwaombe mkae kwa amani na utulivu na mtambue kuwa Serikali ya mama Samia haiwezi kufanya maamuzi ya kuwamiza wananchi" alisema Waziri.

Awali akitoa taarifa ya Wilaya ya Same Mkuu wa Wilaya hiyo Mheshimiwa Kasilda Mgeni alimuomba Waziri kulipatia ufumbuzi suala la Kata ya Ruvu ambayo vijiji vyake vyote vine vipo kwenye Pori Tengefu hivyo wananchi wamezuiwa kufanya uendelezaji katika eneo hilo.

"Mheshimiwa Waziri tuna changamoto ya wananchi wetu wa Kata ya Ruvu kuishi kwenye pori Tengefu,  Wizara ya Maliasili na Utalii ilituarifu kwamba Kata ya Ruvu ni Pori Tengefu lakini Kata hii ina Wananchi elfu kumi na tisa na vijiji vyote vimesajiliwa,hapa kuna shule na kituo cha afya,tunaomba Serikali itusaidie kupata ufumbuzi wa mapema" alisema Mheshimiwa Kasilda.

Mbunge wa Jimbi la Same Magharibi Mheshimiwa David Mathayo aliwaambia wananchi hao kuwa amelazimika kumuomba Waziri wa Ardhi kufika kwenye Kata ya Ruvu ili aweze kusikia kilio cha wananchi hao cha kuzuiwa kufanya maendeleo yoyote katika Kata hiyo hadi Serikali itakapotoa maamuzi.

"Nikuombe tuu Mheshimiwa Waziri haya majibu yaje mapema ili wananchi hawa waache kuishi kwa hofu"alisema Mathayo.

# TUMIENI VEMA MATOKEO YA SENSA KULETA MAENDELEO-RC BABU



*Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu akizungumza na Watumishi wa Halmashauri za Wilaya za Same na Mwanga,Madiwani pamoja na wadau wa Maendeleo wa Wilaya hizo kuhusu matumizi sahihi ya Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022*

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mheshimiwa Nurdin Babu amewataka watumishi wa Serikali na Wadau mbalimbali wa Maendeleo Mkoani Kilimanjaro kuyatumia vema matokeo ya Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2022 katika kuleta Maendeleo.

Mkuu wa Mkoa ameyasema hayo Machi 11 mwaka huu wakati akifungua Semina ya siku moja ya Usambazaji na uhamasishaji wa matumizi ya matokeo ya Sensa ya mwaka 2022 katika Mipango mbalimbali ya maendeleo.

Mheshimiwa Nurdin Babu alisema atahakikisha kuwa matokeo hayo ya Sensa yatatumika vema ili kuharakisha Maendeleo ya Mkoa wa Kilimanjaro katika nyanja mbalimbali.

Matokeo haya yatumike kuweka Mipango Yote Sawa ikiwa ni pamoja na kuhuisha sera ili ziweze kutatua changamoto zilizoainishwa kwenye sensa ya 2022"alisema Mkuu wa mkoa

Alisema kwa mujibu wa matokeo ya Sensa 2022 idadi ya watu kwenye Mkoa wa Kilimanjaro imeongezeka kutoka watu 1,640,087 mwaka 2012 na kufikia watu 1,861,934 mwaka 2022 huku takwimu zikionyesha kwamba Wilaya ya Same ina watu 300,303 ambapo wanaume ni 147,293 na wanawake ni 153,010.

Akizungumza katika Semina hiyo Katibu Tawala wa Mkoa wa Kilimanjaro Bw. Tixon Nzunda alisema Semina hiyo iliyoandaliwa na Shirika la Takwimu la Taifa (NBS) kwa

kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro imejumuisha washiriki zaidi ya 500 kutoka Wilaya za Same na Mwanga.

Alisema washiriki hao ni  Wakuu wa Wilaya,Makatibu Tawala wa Wilaya,Wakuu wa Idara na Vitengo wa Halmashauri ,Madiwani,Watendaji Kata na Vijiji,Wenyeviti wa Vijiji,Viongozi wa Dini na Viongozi wa Vyama vya Siasa.

Alisema lengo la kuwakutanisha wadau hao ni kuwajengea uwezo wa kutumia kwa usahihi matokeo ya Sensa katika kuleta Maendeleo.

## UANDIKISHAJI DARASA LA AWALI NA LA KWANZA WAENDA VIZURI SAME




*Wanafunzi wa Shule ya Msingi Kisima Wilayani Same wakifurahia jambo*

Halmashauri ya Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro, imeandikisha wanafunzi 6,707 wa darasa la awali kwa mwaka 2024 ambapo kati yao Wavulana ni 3,492 na Wasichana ni 3,215 ambapo kati ya hao wenye mahitaji maalum ni 28 wakiwemo wasichana 14 na wavulana 14.

Afisa Elimu ya Awali na Msingi Wilayani Same, Bw. Marclaud Mero amesema idadi hiyo ni sawa na asilimi 83 ya matarajio ya uandikishaji ambayo yalikuwa 8,102.

Akizungumzia uandikishaji kwa darasa la kwanza Bw.Mero alisema Wilaya imefanikiwa kuandiisha  wanafunzi 6,510 , sawa na asilimia 85 ya lengo la uandikishaji ambalo lilikuwa ni kuandikisha wanafunzi 7,638.

Alisema kati ya hao walioandikisha darasa lwa kwanza 20 ni wenye mahitaji maalum wakiwemo 9 wavulana na 11 wasichana.

“Taarifa hizi ni hadi kufikia tarehe 30 Machi 2024 ambapo ndio muda ambao tulifunga zoezi la uandikishaji kwa darasa la awali na darasa la kwanza “ alisema Bw. Mero.

## TAIFISHENI MIFUGO INAYOKULA MITI TUNAYOOTESHA-RC BABU




*Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe.Nurdin Babu*

Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro Mhe. Nurdin Babu, amekemea tabia ya baadhi ya wafugaji kulisha mifugo yao kwenye miti inayopandwa katika maeneo mbalimbali Mkoani humo ambapo ameagiza mamlaka za Serikali kutaifisha mifugo Yote itakayokamatwa ikila miti iliyooteshwa.

Mhe. Babu ametoa onyo hilo Machi 19, 2024 Wilayani Same, Mkoa wa Kilimanjaro wakati akifungua warsha kuhusu masuala ya uhifadhi wa rasilimali za misitu ikiwa ni sehemu ya matukio kuelekea kwenye maadhimisho ya Siku ya Misitu Duniani na Siku ya Upandaji Miti Kitaifa inayofanyika Machi 21 wilayani Same, Kilimanjaro.

"Sisi tunaotesha miti lakini wenzetu.wanakuja kulisha mifugo,naagiza Wilaya zote za mkoa wa Kilimanjaro kutaifisha mifugo yote itakayokutwa inakula miti iliyooteshwa"aliagiza Mhe.Babu

Amesema misitu imekuwa na manufaa mengi na kuwa fursa zake zimekuwa zikiongezeka ikiwamo teknolojia ya hewa ukaa na kuwa wananchi wakizitambua fursa hizo watahamasika katika utunzaji wa misitu kwa ajili ya fursa za kiuchumi.

Misitu inachangia asilimia 3 ya pato la Taifa, inatupatia vifaa vya ujenzi, inasaidia upatikanaji wa mvua,miti inazuia mmomoyoko wa udongo na pia Misitu ni makazi ya wanyama hivyo hatuna budi ya kuhakikisha misitu inahifadhiwa."alisema

Mkuu wa Mkoa alishauri elimu kuhusu umuhimu wa Misitu itolewe kwa wadau mara kwa mara ili kuwezesha utunzaji wa misitu na upandaji Wa miti Kwa wingi.


Naye Mkuu wa Wilaya ya Same, Mhe. Kasilda Mgeni alisema Wilaya ya Same imekuwa ikimuunga mkono Rais Mheshimiwa Rais Dkt. Samia kwa kuhakikisha wanahifadhi mazingira kwa kupanda miti ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Wilaya yetu imezindua kampeni ya upandaji miti ili kuifanya Same ya Kijani na tayari tumepanda miti kandokando ya barabara kuanzia mwanzo hadi mwisho wa wilaya na mpaka sasa zaidi ya miti laki tano imeshapandwa"alisema Mkuu wa Wilaya.

Akizungumza katika hafla hiyo, Kaimu Mkurugenzi wa Maendeleo ya Ufugaji Nyuki, Bw. Daniel Pancras amesema Serikali kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii inajukumu kubwa la kuhamasisha upandaji miti pamoja na kuelimisha juu ya upandaji miti ili watanzania wajue namna bora ya kupanda na kutunza miti.

## SAME YAPATA MKURUGENZI MPYA

- **NI JIMSON MHAGAMA**
-



*Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Bw.Jimson Mhagama*

Halmashauri ya Wilaya ya Same imepata Mkurugenzi Mtendaji mpya Bw. Jimson Mhagama kufuatia mabadiliko ya wakurugenzi watendaji yaliyofanywa na Mheshimiwa

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan Machi 09 mwaka huu.

Mkurugenzi Mhagama amehamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Same Mkoani Kilimanjaro akitokea Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni, Singida ambapo wamebadilishana kituo cha kazi na aliyekuwa Mkurugenzi Mtendaji wa Same Bi. Anastazia Tutuba aliyehamishiwa Manyoni, Singida

Bw. Mhagama pia aliweza kukutana na kufahamiana na wajumbe wa Timu ya Menejimenti ya Halmashauri (CMT) ya Wilaya ya Same na kupanga mikakati ya uendelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo Wilayani humo.

## WAKULIMA WA TANGAWIZI WAOMBA SERIKALI KUWATAFUTIA MASOKO



*Mwenyekiti wa Ushirika wa Wakulima wa Tangawizi Kata ya Myamba Bw. Mbaraka Ali*

Wakulima wa Tangawizi Wilayani Same wameiomba Serikali kuwatafutia masoko ya nje ya nchi ili kuwasaidia wakulima kuwa na soko la uhakika la zao hilo.

Wakizungumzia hali ya soko Wakulima wa Kata za Mpinji na Myamba wamesema kuwa soko la zao hilo limekuwa sio la uhakika hivyo wakati mwingine wamejikuta wakiuza tangawizi kwa bei ya chini sana.

Mbaraka Ali ni Mwenyekiti wa Ushirika wa Wakulima wa Tangawizi Kata ya Myamba amesema kuna haja ya Serikali kuingilia kati na kusaidia wakulima kutafuta soko la zao hilo.

“Inafika wakati tunauza Tangawizi mbichi kilo moja shilingi mia sita wakati bei inatakiwa kilo moja kuuzwa kwa shilingi elfu mbili ndio itakayomwezesha mkulima kupata faida” alisema Bw. Mbaraka

Mwenyekiti huyo anamshukuru Mbunge wa Same Mashariki Mhe. Anne Killango Malecela kwa kuwezesha kuanzishwa kwa Kiwanda cha kusindika Tangawizi cha Myamba ambacho kimekuwa msaada pia kwa wakulima.

Alisema uwepo wa Kiwanda umeongeza upatikanaji wa soko lakini bado kiwanda kinanunua Tangawizi kulingana na bei iliyopo sokoni ambayo haijawahi kuzidi shilingi 1,200 kwa kilo moja.

Nae Afisa Masoko wa Kiwanda cha Tangawizi Myamba Bw. Venance Manjati anaungana na Mwenyekiti wa Ushirika wa Wakulima Bw.Mbaraka kuomba Serikali kuwatafutia Masoko ya uhakika.

“Hali ya soko la Tangawizi sio nzuri,tunaomba Serikali itusaidie kutafuta masoko ya nje au ituwezeshe kwenda nje kutafuta masoko,tangawizi inayozalishwa Same ni tangawizi bora sana hivyo haipaswi kukosa soko”alisema Bw.Manjati

Akizungumzia hali ya uzalishaji kwenye Kiwanda hicho kinazalisha tani 30 za Tangawizi kwa mwezi ambzo huuzwa kwa wateja wa ndani ya nchi ambapo kilo moja ya Tangawizi iliyosagwa huuzwa kwa shilingi 15,000/-



*Afisa Masoko wa Kiwanda cha Tangawizi Myamba Bw. Venance Manjati*

# WFP KUFADHILI MRADI KIJIJI CHA SAWENI




*Aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya Bi. Anastazia Tutuba akiongoza wananchi katika mjadala wa kuibua Miradi ili Shirika la Chakula Duniani (WFP) liwezeshe,kushoto kwake ni Mratibu wa Miradi ya WFP nchini Bw.Elisha Moyo na Diwani wa Kata ya Saweni Bw.Elieskia Mwalili  na kulia kwake ni Afisa Kilimo wa Mkoa wa Kilimanjaro Bw.Godwin Maro.*

Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) linatarajia kuendesha Mradi shirikishi kwa wananchi wa Kijiji cha Saweni Wilayani Same ili kuwezesha wananchi hao kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.

Wawakilishi kutoka Wizara mbalimbali na mafisa kutokaShirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP)walifika kuzungumza na wananchi wa Kijiji cha Saweni ili kufahamu mahitaji yao ambayo yatawezesha utekelezaji wa Mradi huo ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa miaka mitano katika Kijiji hicho.

Akizungumza katika kikao hicho Mkazi wa Saweni Bw. Elikunda Mseli aliomba WFP kufanya utafiti wa mbegu zinazohimili ukame ili waweze kuwagaia.

“Tunaomba tafiti zifanyike ili kujua mazao yanastahamili ukame ili tuweze kugaiwa lakini pia tujengewe maghala ya kuhifadhi chakula” Alisema Mseli

Nae Bi Aziza Ally ambaye ni Mkazi wa Kijiji cha Saweni aliomba WFP kuwajengea mabwawa ya maji kwaajili ya umwagiliaji.

“Kila mwaka tunalima lakini hatuvuni maana tunategemea maji ya mvua na yakija yanapita tu,hivyo tunaomba tujengewe mabwawa ya kuvuna maji ya mvua” alisema Bi. Aziza.

Akizungumza na wananchi wa Kijiji cha Saweni Mratibu wa Miradi wa WFP nchini Tanzania Bw.Elisha Moyo alisema wamefika kijijini hapo kama hatua ya mwanzo ya kusikiliza mahitaji ya wananchi ili kuyachambua na kuanzagalia viapaumbele vya kuanzia.

Alisema Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) limeanza kufanya upembuzi yakinifu kwenye Kijiji cha hicho kwa lengo la kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi kwenye upatikanaji wa chakula.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same,Bi Anastazia Tutuba alilishukuru shirika la WFP kukichagua Kijiji cha Saweni katika kutekeleza Mradi huo na ameahidi kutoa ushirikiano katika kuhakikisha kuwa malengo yanatimia.

## VIONGOZI WAENDELEA KUSISITIZA SMK IKAMILIKE JUNI 2024



*Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2024 Ndg. Godfrey Mnzava, akizungumza na wananchi wa Same wakati Mwenge wa Uhuru ukiwa Wilayani Same April 08,2024*

Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru Kitaifa Ndg.Godfrey Mnzava ameagiza Wizara ya Maji kuhakikisha kuwa Mradi mkubwa wa Maji wa Same-Mwanga-Korogwe (SMK) unakamilika ifikapo mwezi Juni 2024 kama alivyoagiza Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango.

Kiongozi huyo alitoa agizo kufuatia ombi la Mbunge wa Same Magharibi Mhe.David Mathayo ambaye aliwakilisha changamoto ya upatikanaji wa Maji ya uhakika kwa wakazi wa Same.

"Tunashukuru tangu alipofika Makamu wa Rais Mhe.Philip Mpango tumechimbiwa visima kadhaa ambavyo vimesaidia kwa kiasi kupunguza changamoto ya Maji, lakini bado tunahitaji Maji ya kutosha"alisema Dkt Mathayo.

Kufuatia maombi hayo Kiongozi wa Mbio za Mwenge 2024 Ndg Mnzava aliagiza Mradi mkubwa wa Maji wa SMK kukamilika mwezi Juni 2024 kama alivyoagiza Makamu wa Rais Mhe.Philip Mpango.

Mwenge wa Uhuru umewasili Wilayani Same April 8 na umeweka jiwe la Msingi kwenye Mradi wa Ujenzi wa Barabara Km 1.4 za kiwango cha lami nyepesi ambayo imegharimu shilingi milioni 980.9.

Mwenge wa Uhuru ulitembelea Kituo cha watoto wenye mahitaji maalum cha Mother Kevina kilichopo Kata ya Kisima ambacho kinalea watoto 44 wakiwemo watoto wadogo wa Shule za Msingi, Sekondari na wa vyuo.

Kwenye Kituo cha Mother Kevina Kiongozi wa Mwenge wa Uhuru Ndg.Mnzava amekabidhi hundi ya shilingi milioni tatu fedha zilizotokana na michango ya Mwenge kwaajili ya kuwezesha ununuzi wa viti mwendo viwili.

Mwenge wa Uhuru umetembelea pia Kikundi cha Wajasiriamali cha Wandeme ambacho kinajishughulisha na kutengeneza samani za majumbani na za Ofisini.

Kikundi hicho kina mtaji wa milioni 10 na kilipatiwa mkopo wa milioni mbili kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Same.

Miradi mingine iliyofikiwa na Mwenge wa Uhuru 2024 ni Mradi wa Kitalu cha Miti cha Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) ambao umegharimu Tsh.79,049,000/-

Mwenge wa Uhuru 2024 umezindua pia Klabu ya Wapinga Rushwa Shule ya Sekondari Makanya.

Ukiwa Wilayani Same Mwenge wa Uhuru ulizindua Mradi wa Maji wa Kijomu- Mabilioni ambao umegharimu shilingi milioni 447.7Mradi wa Maji Kijomu-Mabilioni umesaidia kuondoa kero ya upatikanaji Maji kwa zaidi ya wananchi 2,000

Mwenge wa Uhuru ulizindua jengo la mama na Mtoto kwenye Kituo cha Afya Hedaru, jengo ambalo Ujenzi wake umegharimu shilingi milioni 528 ambapo milioni 8 kati ya fedha hizo zinatokana na nguvu za wananchi.

Katika Wilaya ya Same Mwenge wa Uhuru umefikia Miradi nane yenye thamani ya Tsh.Bil.3.6

Baada ya kukamilisha ziara yake Wilayani Same, Mwenge wa Uhuru ulikabidhiwa Mkoani Tanga April 9 katika eneo la Mazinde.

Kaulimbiu ya Mwenge wa Uhuru 2024 "Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu"

## MATUKIO MBALIMBALI KATIKA PICHA



*Mbunge wa Same Magharibi Dkt.David Mathayo akisisitiza jambo kwa Kiongozi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru 2024 Ndg.Godfrey Mnzava*




*Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni akimkabidhi taulo za kike mwanafunzi wa Shule ya Sekondari Kwakoko kwa niaba ya wenzie kama sehemu ya maadhimisho ya siku ya wanawake Duniani mwaka 2024.Taulo za kike zenye thamani ya shilingi milioni moja ziligawanywa kwa wanafunzi wa shule hiyo na shule ya sekondari Mighareni.*



*Mkuu wa Wilaya ya Same Mheshimiwa Kasilda Mgeni akipokea Mwenge wa Uhuru 2024 kutoka kwa Mkuu wa Wilaya ya Mwanga Mheshimiwa Abdallah Mwaipaya .*



*Mbunge wa Same Mashariki Mheshimiwa Anne Kilango Malecela akitazama daftari la mwanafunzi alipofika kutembelea shule mpya ya msingi ya kisasa (shule salama) ya Anne Kilango iliyopo Kijiji cha Mgandu Kata ya Bendera.Shule hiyo imejengwa kwa gharama ya shilingi Milioni 348.5 fedha kupitia Mradi wa BOOST.*




*Wananchi wakifuatilia matukio mbalimbali kwenye Tamasha la Same Utalii Festival*



*Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Same Bw. Jimson Mhagama (kushoto) akimkabidhi mpira Mwl.Rafael Justine wa shule ya Sekondari Same kwaajili ya kuendeleza michezo mashuleni,anayetazama katikati ni Afisa Elimu Msingi Bw. Marclaud Mero.Wilaya ya Same imepokea jumla ya mipira 130 kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Nchini (TFF) kwaajili ya kuendeleza michezo mashuleni, Mipira hiyo imegawanywa kwa shule 19 za Msingi na Sekondari.*



*Aliyekuwa Katibu wa NEC Itikadi, Uenezi na Mafunzo wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bw. Paul Makonda akizungumza na Wananchi wa Same alipofanya ziara Wilayani Same, Makonda kwasasa ni Mkuu wa Mkoa wa Arusha.*




JARIDA MTANDAO LA HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

LIMEANDALIWA NA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI

S.L.P 138,SAME

Mhariri wa Mkuu: Jimson Mhagama

Mhariri wa Habari: Amina Sangawe

*Machi 2024 www.samedc.go.tz email: ded@samedc.go.tz Same DC samedc2022*